TOLEO NO.65

# Khilafah

SAFAR 1447 HIJIRIA — AGOSTI 2025 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

TOLEO MAALUM

## CHANZO NA MALENGO YA FIKRA YA HATARI YA 'DINI MSETO'




Mtume SAAW na makhalifa baada yake waliubeba Uislamu kiukamilifu ukiwa ni haki kutoka kwa Mola wao bila ya kuchanganya haki hiyo na batil, kinyume na inavyopigiwa debe leo kwa kampeni batil ya dini mseto'.


Harakati hizi za 'dini mseto' zinazomaanisha kuleta ukuruba baina ya dini zilianza rasmi 1932 pale Ufaransa ilipotuma wawakilishi wake Chuo Kikuu cha Azhar ili kuasisi ukuruba baina ya Uislamu, Ukristo na Uyahudi.

Moja kati ya malengo makubwa ya fikra hii ya 'dini mseto' ni kutaka kuzuiya sheria za dini kutawala duniani. Na badala yake fikra ya 'dini mseto' inapigiwa debe kutawalisha sheria za kibepari na kidemokrasia zinazotokamana na akili finyu ya wanadamu kupitia mabunge. Yawe mabunge ya Marekani, Ulaya au nchi vibaraka ambazo baadhi tayari yamesharuhusu uovu mwingi kama ushoga, ulevi, utoaji mimba, kodi za kuuwa maskini nk.

Aidha, harakati za 'dini mseto' zinalenga kulaani na kuzuiya fikra ya dini yoyote kuwa na sheria na utawala, kwa hoja dhaifu

**Inaendelea Uk. 3**

## SABABU ZA KUZUKA HARAKATI ZA KUPINGA DINI




Katika historia ya waanadamu wamekuwapo watu kibinafsi ambao walikanusha uwepo wa Mungu Muumba kutokana na kiburi chao au kulinda maslahi fulani, pamoja na ukweli kuwa upingaji wa uwepo Muumba ni jambo lisilokinaisha akili.

Hata hivyo, ukanushaji uliopo sasa baada ya kusimama mfumo wa kibepari ni ukanushaji uliochukua sura rasmi ya kimfumo, taasisi na kiharakati unaolinganiwa, kulindwa na kuendelezwa

kwa sera na mikakati maalum, tena kilimwengu.

Kwa karne nyingi zama za giza za Ulaya zinazoitwa 'Middle ages' au 'Medieval period', bara hilo lililikua likitawaliwa kwa ukabaila (feudilism) chini ya tawala za kifalme, wasaidizi watukufu wa wafalme (nobility) na makasisi wa kanisa. Tawala hizi zilikuwa na nguvu kubwa kiasi kwamba wanahistoria wa Ulaya wakazipachika jina la 'Absolute Monarchy (falme zenye kuhodhi mamlaka yote ). **Uk .2**

### Yaliyomo :


- **Kampeni ya Kulinda Aqida Yachanja Mbuga.... ...uk.2**
- **Hoja za Uwepo wa Mwenyezi Mungu.................uk.5**
- **Amali za visimamo na mabango........................uk.8**

# KAMPENI YA KULINDA AQIDA YA KIISLAMU YACHANJA MBUGA

Mwanzoni mwa mwezi wa Muharram 1447 Hijria (27 Juni 2025) Hizb ut Tahrir Tanzania katika Masjid Rahma, Buguruni, Dar es Salaam ilizindua kampeni maalumu ya kitaifa ya kulinda na kutetea Aqida ya Kiislamu.

Kampeni hiyo ya miezi miwili ya hijria inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu wa Saffar 1447 Hijria.

Dhamira kuu ya kampeni hiyo ni kuilinda na kuitetea Aqeeda ya Kiislamu kwa kumakinisha ufahamu Sahihi wa Aqeeda ya Kiislamu kwa upana wake. Hali hii ni kutokana na kuenea, kusambaa na kupigiwa debe fikra za kipotofu ambapo harakati za kusambaza fikra hizo hudhaminiwa na madola ya magharibi ya kibepari huku lengo lao kuu nyuma ya pazia ni kupambana na Uislamu, kutia shaka Waislamu na dini yao, kuvuruga mshikamano baina ya kijamii, kuwaongeza chuki wasiokuwa Waislamu wauchukie zaidi Uislamu.

Kutokana na fikra hizo kuchukuwa sehemu kubwa katika mijadala hususan katika mitandao ya kijamii, kampeni imebeba Kauli Mbiu ya: "Kataa Dini Mseto, Ukristo, Upagani, Mizimu, baki na Uislamu"

Kwa kipindi cha mwezi mmoja wa kampeni licha ya changamoto ndogo ndogo kwa kutumia mbinu mbalimbali kama uandishi wa makala, mihadhara, khutba za Ijumaa, visimamo vya mabango, mitandao ya kijamii nk. kampeni imeendelea vyema kuwafikia Umma kwa kuzikosoa




fikra hizo batil na kutandika ufahamu sahihi wa Kiislamu.

Wakati tukiwa nusu ya pili ya kampeni hiyo inatupasa kukaza kamba zaidi kuhakikisha kwamba kampeni hii inafikia wengi na mbali zaidi ili kuinua ufahamu sahihi kwa Waislamu kwa kuwatanabahisha juu ya hatari ya fikra thakili dhidi ya Uislamu, bali pia kuwafahamisha na kuwazindua wasio kuwa Waislamu kwamba fikra na mitizamo hiyo ya upagani, dini mseto na dini za kiafrika sio tu ni tishio kwa Uislamu na Waislamu bali ni hatari dhidi ya ubinadamu na ustawi wa jamii kwa jumla.

Katika kumalizia nusu ya pili ya kampeni hii, tunawataka Waislamu wazidishe ushiriki wao katika kampeni hii ya kupambana katika vita hivi hatari vya kifikra hususan katika maeneo yafuatayo:

1. Waislamu wajitahidi zaidi kuifutilia kampeni hii na kuonesha mashirikiano kwa kushiriki amali mbali mbali zinazoendelea kitaifa.
2. Waislamu wasaidie kufanikisha kupatikana mijadala ya wazi na ya kistaarabu dhidi ya wanaoshikilia fikra hizo hususan upagani na dini za jadi.
3. Waislamu wazidishe ushiriki wao katika mitandao ya kijamii dhidi ya wafuasi wa fikra hizo hatari, ambapo watu hao hutumia zaidi majukwaa hayo kufikishia fikra zao.

**Mwisho**, **Hizb ut Tahrir Tanzania** inawashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika nusu safari ya kampeni hii, huku tukiwakumbusha wao na Waislamu jumla kwamba bado kampeni inaendelea kwa mwezi mmoja.

Hivyo, tunatoa mwito kwa Waislamu, wanajamii katika waadilifu waendelee kushirikiana nasi kikamilifu kuinogesha na kuifanikisha kampeni dhidi ya fikra hizo hatari, fikra ambazo sio tishio tu kwa Uislamu na Waislamu bali kwa ubinadamu na ustawi wake.

**Mhariri**

**Safar 1447 Hijria**

**Agosti 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

## Upagani- Kutoka Uk 1

Taasisi mbili hizi (utawala wa kifalme na kanisa katoliki) zilikua zikifanya kazi bega kwa bega katika kuwadhulumu, kuwatesa na kuwadhililisha raia. Kanisa kwa upande wake likihalalisha uwepo wa utawala uliotamalaki na dhulma zake katika kodi, tozo mbalimbali, adhabu za kishenzi hadi mauaji ya kikatili hadharani kwa wanaopinga tawala hizo nk.

Msimamo wa kanisa ukawa wazi kwa wananchi kwa kuwaeleza ... **uk. 4**

## Chanzo na malengo ya fikra ya hatari ya 'Dini mseto'... *Kutoka uk .1*

kuwa dini zitaleta fujo na maafa duniani. Ilhali maafa, mauaji, mateso na vita visivyokwisha duniani leo na vilivyotangulia vimesababishwa na ubepari na demokrasia yake na wala sio dini.

Hata pale kunapokuwa na vita vinavyojidhihirisha kuwa vya kidini, mara nyingi kama sio zote, kwa leo madola ya kibepari ndio waasisi wa vikundi vingi kwa malengo maalumu, na pale wanapoona wavimalize vikundi hivyo, huviangamiza. Basi kwanini wanaolingania fikra hizi wasingelaani mfumo huu wa kibepari wenye maafa, badala yake wanapambana na kitu ambacho wanakhofu tu ikiwa kitapatikana kitaleta maafa? Mbona wanajitia upofu katika jambo lililolowazi?

Malengo hayo ya'dini mseto' ya kuhubiri sheria za kidini zisiruhusiwe kumuongoza mwanadamu madamu tu kwa kuwa dini zingine hazina sheria za siasa na kiutawala sio tu ni hoja dhaifu, bali ni wazi kuwa hapa mlengwa mkuu ni Uislamu, kwa kuwa ndio dini pekee yenye sheria na miongozo katika nyanja ya utawala. Na mchakato wa harakati hizi zina dhamira ya kuangamiza kijanja kwa kuonesha dini mseto wanakabili dini zote.

Uislamu haukubali kamwe kuhoji sharia zake, bali hauruhusu kabisa kushirikiana na dini zingine katika mambo ya kiimani na kidini. Bali Uislamu unaruhusu Waislamu kushirikiana na wasiokuwa Waislamu katika miamala binafsi ya kijamii na kiuchumi kama ujirani, biashara, kusaidiana nk. Lakini sio kuungana kidini na kiimani na watu wa dini zingine, kama tunavyoona leo baadhi ya masheikh wakiingia makanisani na baadhi ya maaskofu kuingia misikitini.

Sisi katika Uislamu tunaamini kuchanganyishiwa Imani yetu na Imani nyengine huo ni ukafiri. Na msimamo huu wa kutoshirikiana kiimani pia upo hata kwa dini zingine zisizokuwa Waislamu. Mathalan, kamwe hutosikia makanisa yakipiga marufuku kula nguruwe ili kuungana na Waislamu, japo tunaona wakristo na Waislamu wakisaidiana kwenye matatizo yao. Basi vipi Muislamu anayeamini Mungu Mmoja, hakuzaa wala kuzaliwa kuungana na mtu anayeamini Mungu alizaa au alizaliwa, alikufa bali alicharazwa viboko kamwe? Hawawezi watu kuungana isipokuwa pale mmoja atakapoacha dini yake na kufuata ya mwingine.

Enyi Waislamu! mabepari wameshindwa kumletea mwanadamu ufanisi, furaha na amani ya kweli, ndio maana wanamtafutia mwanadamu amani ya kufikirika kupitia 'dini mseto'. Kwa bahati mbaya, baadhi ya madalali wa kampeni hii pia wamo Waislamu ili iwe rahisi kuwarubuni watu wa kawaida.

Tunawazindua Umma juu ya hatari, fitna na balaa la 'dini mseto'. Aidha, tunawadharisha Waislamu na wanadamu kwa jumla juu ya amani ya kufikirika, huku wafadhili wa kampeni hiyo ya 'dini mseto' wakiendelea kuwarundika Waislamu magerezani kwa dhulma, mateso na kumwaga damu zao kila mahala.

Basi simamaeni imara enyi Waislamu kuifedhehi na kuikosoa vikali fikra hii ya hatari na ya kikafiri. Tunawalingania na kuwaita kwa ikhlasi Waislamu kuja katika uwajibu wa kurejesha tena dola ya Kiislamu ya Khilafah itakayodhamini kuulinda Uislamu na kila adui wa kivitendo au kifikra

****

## BAADHI YA MATUKIO YA SWAFAR

1. Jaribio la makafiri kumuuwa Mtume SAAW. Viongozi wa makureish walikutana kujadili ajenda ya hatari kwa kuchagua kijana mmoja kutoka kila kabila la kikureish ili vijana hao kwa pamoja washirikiane kumuuwa Mtume SAAW. (26 Saffar, Mwaka wa 14 wa Utume)

2. Ghazwatu al- Abwa /Waddan

Kwa mara ya kwanza tangu Mtume SAAW asimamishe dola aliiongoza kikosi cha watu 70 kwa lengo la kudhoofisha uchumi wa Makureish na kuandaa mazingira ya vita dhidi yao (2. AH kabla ya Vita vya Badr)

3. Sarriya ya Aban bin Said

Kikosi hiki kilitumwa kwenda Najd kuwatia khofu mabedui wa huko, kiliporudi Waislamu tayari wameshaifungua Khaybar (Mwaka wa 7AH)

watu kwamba tawala hizo na matendo yake ni 'chaguo la Mungu' (divinely) na wananachi viwe viwavyo wana wajibu wa kunyenyekea utawala na kutii, kwa kuwa hilo ni mpango wa Mungu uliokwisha kadiriwa (predestined)

Wakati Ulaya ilipokuwa ikitoka kutoka zama za giza kwenda katika zama zinazoitwa za kuhuika (renaissance) kuanzia karne ya 14 -17, zama zilizoambatana na ubunifu na uvumbuzi, kanisa sio tu lilipinga vikali baadhi ya uvumbuzi wa kisayansi, bali kuwaadhibu na kuwanyanyasa wavumbuzi wake.

Kwa mfano, mwaka 1633 mvumbuzi mtaliano, Galileo alipotamka kuwa dunia inazunguuka, aliitwa na kuwekwa kiti moto mbele ya Papa Urban VIII kuhojiwa na kutishwa, kwa kuwa mtazamo huo wa Galileo ulikuwa unapingana na mtazamo wa miaka 1000 uliokalidiwa/ kushikiliwa na kanisa.

Hatimae mwanasayansi Galileo akawekwa katika kifungo cha nyumbani (house arrest) na akafariki mwaka 1642.

Ndani ya mwaka 1992 Kanisa Katoliki likaomba radhi na kutambua Galileo alikuwa sawa katika uvumbuzi wake.

Kilipofika kipindi cha zama zinazoitwa za 'Mwamko' (enlightment era) ndani Ulaya mwishoni mwa karne ya 17 mpaka karne ya 19, kipindi kulichoibuka wimbi kubwa la wanafalsafa, wanafikra, wasomi na wanamageuzi waliokuja na fikra za 'uhuru' za kidemokrasia

ambazo zilileta 'amsha amsha' na vuguvugu na kuungwa mkono na wanachi hadi kupelekea mapinduzi ndani ya Ulaya kwa kuanzia Ufaransa mwaka 1789 na kumakinishwa na kutabikishwa mfumo wao wa kibepari, aqida yake 'usekula' na nguzo zake za 'uhuru'

Fikra ya usekula ikapelekea wanamapinduzi na makasisi kuvutana kuhusu nafasi ya dini katika mchakato wa mageuzi haya ya kisiasa. Hatimae walifikia suluhisho la kati na kati (compromise), suluhisho la kufanya kila upande kuondoka na 'chochote kitu'. Ikawafikiwa kwamba makasisi wabakie na dini yao (ukiristo) lakini imalizie katika majumba ya ibada pasi na kuwa na usemi au ushawishi wowote katika maamuzi ya nchi, na wanamageuzi na wanamapinduzi

wasimamie na kuratibu mambo ya utawala na uendeshaji wa nchi kwa matakwa ya wananchi.

Kwa suluhisho hili japo dini haikukanushwa wazi lakini ni kejeli ya wazi ya na dharau kwa dini, na lilisukumwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo jumla wa kuchukia dini. Na zaidi 'fikra ya uhuru wa kuabudu' ambayo ni katika mihimili ya mfumo mpya wa wanamageuzi ambayo inalifanya suala la uwepo Mungu sio jambo muhimu, anaweza mtu kuamini au kuacha.

Haya yote yanatoa sura ya ushindi mkubwa kwa wanamageuzi katika kudhihirisha athari ya kuchukia kwao dini, kuidharau, kuibeza nk.

Takriban wanafikra na wasomi wote wa zama za Mwamko (enlightment) kama muingereza John Locke (1632) katika maandishi yake 'Two treatises of government', Charles Montisquieu (1689) katika fikra zake za 'Separation of power' (mgawanyo wa madaraka), Jacques Rousseau (1712) katika kitabu chake cha 'The Social Contract' nk. wanakubaliana juu ya kuwapa watu mamlaka yao ya kujiamulia mambo yao, ikiwa na maana kuidharau dini na kupinga kanisa kupewa nafasi. Mbali ya kundi la wanafikra walioona ukiristo ubakishwe lakini kuwa jambo la kibinafsi kando na masuala ya uendeshaji nchi. Pia kundi jengine la wanafikra kama Baron D'Holbach (1713) na Denis Diderot na (1723) wakaikanusha dini kamwe!

Kwa hivyo, wanafikra hao wakatoa msukumo mkubwa kwa watu wa Ulaya kuchukia dini, na mtazamo huo ukashikiliwa na wanachi wengi ndani ya Ulaya.Uzoefu wa wanafikra na wanamageuzi na watu jumla wa Ulaya juu matukio maovu yaliyotendwa na wafalme kwa mashirikiano na kanisa, na pia yaliyotendwa na kanisa binafsi, kudhulumu mali za raia kupinga kwao uvumbuzi wa kisayansi ambao baadae ulikuja kuthibitishwa, kuwatesa na kuwaua walioasisi madhehebu mapya kutoka katoliki, yote hayo yalisaidia kuongeza rutba ya wanamageuzi kuungwa mkono na Umma juu ya kuichukia dini (ukiristo) na kutia shaka mafunzo ya biblia na kufanikisha mapinduzi yaliyomakinisha itikadi ya usekula.

Karne ya 18 na 19 ni kipindi **Uk...8**

# HOJA ZA KIAKILI JUU YA UWEPO WA MWENYEZI MUNGU

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la watu wanaodai kukanusha uwepo wa Mungu Muumba wa Kila kitu. Aidha fikra hizi ni kongwe katika Ulaya na zimeanza kuenezwa kwa kasi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.

Chanzo cha fikra hizi ni Ulaya ya Magharibi ambapo baada ya kushuhudia dhulma kubwa na unyonyaji uliofanywa na mabwenyenye kwa kusaidiwa na kiasi kikubwa na kanisa katoliki walianza kuchukia na kupuuza dini na fikra ya uwepo wa Mungu katika maisha yao.

Fikra hizi zikashika hatamu karne ya 18 hususan baada ya Mapinduzi ya Ufaransa yaliyokuja baada ya mapinduzi ya Uingereza. Mabadiliko makubwa ya kuondoa dini katika utawala na maisha yakatokea, na taratibu baada ya kukomaa ubepari kutokamana na mfumo wa ukabaila, na huo ubepari na ukiristo baada ya kushindwa kutatua matatizo ya binadamu, uliibuka mfumo mpya wa Ujamaa ambao wenyewe ndiyo uliweka wazi itikadi yake ya kukana uwepo wa Mungu.

Hata baada ya kuanguka ujamaa katika karne ya 20 na kuvunjika kwa Umoja wa kiSovieti mwaka 1991 tayari jamii kubwa ya Ulaya ilikuwa imeathirika na fikra hizi zisizo



na msingi wowote.

Kufuatia hali hii kuendelea na kuathiri sehemu kubwa ya ulimwengu kwa sasa tumeleta hapa baadhi ya hoja za kiakili tu zinazofidisha juu ya uwepo wa Mungu Muumba, Mwenyezi Mungu, Allah Taala.

Ni kinyume na uhalisia kukataa uwepo wa Mwenyezi Mungu

Fikra na uhalisia ni vitu vinavyoenda sambamba. Fikra hutumika kuelezea uhalisia wa jambo, na pindi fikra inapoonekana kuwa kinyume na uhalisia, hapo huwa fikra hiyo si sahihi.

Fikra kuwa viumbe vyote viliibuka tu kutokana na mada bila ya kuwa na Muumbaji yaani Mwenyezi Mungu kama ilivyosemwa na Karl Marx ni fikra inayopingana na uhalisia. Fikra hii si sahihi na inapingana na uhalisia kwa sababu mada ni kitu halisi ambacho uwepo wake lazima kuwepo kwa chimbuko (chanzo) lake. Kwahiyo, ni wazi kuwa hii mada inayosemwa kuwa ndiyo chanzo cha uhai na viumbe, yenyewe pia ni kiumbe na ina chanzo chake, jambo ambalo wameshindwa kulielezea wanaopinga uwepo wa Mwenyezi Mungu.

Kila kiumbe ni tegemezi

Kila chenye kudhihirika huwa ni tegemezi. Kwahiyo viumbe vyote ni dhihiriko lililo na utegemezi kwa Muumba wao. Hivyo ,amejikuta binadamu akiwa ni mtegemezi mwenye udhaifu, na hii ndiyo hali ya viumbe wote huhitaji nguvu nje yao kuishi. Hii inaonesha wazi kuwa yupo mtegemewa wa viumbe wote ambaye ndiye anayeamua umri wao wa kuishi, namna yao ya kuishi, nk. Kila kiumbe kina chanzo na hakuna kitu kinapatikana tu kwa bahati mbaya.

Baada ya kuwa viumbe na wanadamu huchukua sura ya kuwa ni tegemezi, ni wazi kuwa kila kinachotegemea kina chanzo chake (source and effect). Akili ya mwanandam inalazimisha uhalisia kuwa kitu chochote na uhalisia wowote (reality/effect) kwa kufuatilia sababu (reasoning) huwa kina chanzo chake (source).

Kwahiyo, kwa kutumia kununi hii, ni wazi kuwa viumbe vyote vina chanzo chake na ni tegemezi juu ya chanzo hicho, na huwa ni kinyume na uhalisia kukataa ukweli huu. Hii ni hoja inayoonesha kuwa Mwenyezi Mungu yupo na ndiye chanzo na mtegemewa wa kila kitu.

Udhaifu wa sayansi katika kufikiria uwepo wa **Inaendelea uk...7**

Kampeni maalumu ya 'Dini Mseto', yaani ukuruba wa kidini baina ya Waislamu na makafiri inaendelea kushamiri na kupamba moto. Miongoni mwa mawazo duni yanayoambatana na fikra hii ni mawazo ya 'Dini za Kiafrika', Imani za KIijadi au Imani za Mababu.

Watu wa Imani za kijadi wanapaza sauti zao kutaka watu warudi kwenye Imani za asili za mababu zao. Lakini cha kushangaza waumini hao wa dini za mababu hawana uwezo wa kuthibitisha madai yao kwamba imani zao hizo ni sahihi na zinamfaa mwanadamu, hasa mwanadamu anayetaka mabadiliko kutoka hali duni kwenda katika hali nzuri ya ustawi wa maisha yake hapa duniani.

Madai makubwa ya waumini wa dini za kijadi yamesima kwenye mtizamo kuwa kufuata Uislamu ni kudharau mababu zao na mila za mababu. Aidha wanadai kuwa Uislamu ni imani iliyoletwa na waarabu na haituhusu sisi. Pia wanitilia mkazo madai yao kuwa kabla ya Uislamu Afrika tulikua tukiomba mizimu tunajibiwa, na tulikua na maendeleo. Bila ya kusahau hoja yao kuwa Uislamu umefuta hata majina yetu ya asili, umeleta vita, vurugu, utumwa, ukoloni nk.

Hizi ndiyo baadhi ya hoja zao, japo katika madai yao hayo hutaja na kuzungumzia dini zote kama ukristo nk. Lakini tutagusia upande wa Uislamu zaidi, kwavile licha ya ya Waumini wa Imani za jadi kuzungumzia dini nyingine, lengo na shabaha yao kuu ni Uislamu.

Kabla ya kuingia moja kwa moja katika kujibu hoja zao ni vyema ifahamike kuwa madai yao haya yana msingi wa dhulma na chuki, na chuki zao dhidi ya dini zimewafanya kuacha kutofautisha kwa makusudi baina ya Uislamu na dini nyingine, licha ya kujua kuwa misingi, miiko na maadili ya Uislamu ni tofauti na dini nyingine.

Pia watu hao wamechanganyikiwa kiasi cha kushindwa kuweka wazi Uafrika wanaotetea ni kitu gani? Je ni rangi nyeusi au eneo la bara la Afrika? Kama ni rangi basi kuna watu wenye rangi nyeusi wa asili wapo Arabuni, India, Australia nk. Na kama ni bara, basi bara la Afrika kuna waarabu wengi na wanazungumza kiarabu kama Misri, Sudan, Tunisia, Morocco nk.

Hivyo, mpaka hapa imekua madai yao haya hayana mashiko na ni wazi hawajui nini wanapinga na nini wanataka.

Majibu yetu ya hoja zao dhaifu ni kama ifuatavyo:

Kwa kuanzia na hoja ya kudharau mababu. Katika hili Uislamu umekuja kuwaweka wanadamu wote sawa, waarabu na wasiokuwa waarabu. Mababu wote wamepewa heshima sawa, na mababu wote ambao wameacha mafundisho sahihi ya Muumba hao watakua wamejiweka katika kundi duni wao wenyewe.

Kwahiyo, Uislamu haujainua mababu wa kiarabu na kuwatupa mababu wa kiafrika, kwani tunaona kuwa miongoni mwa mababu wakubwa wa kiarabu kama Amru Ibn Hisham (Aabu Jahl), yeye sio tu alikuwa katika mababu wa kiarabu bali alikuwa kiongozi wa waarabu (makureishi) na mtu anayeheshimika sana, Uislamu ulimdhalilisha kwa ukafiri wake. Bila ya kusahau mababu wengine wa kiarabu kama Abu Lahab, Walid Ibn Mughira nk. ambao Uislamu uliwazungumza kwa ukali kaisi cha kutangaza maangamizi ya baadhi yao ndani ya kitabu chake cha Quran.

Kwa upande mwingine, Uislamu ukawainua na kuwaheshimisha mababu kutoka jamii ya kiafrika na jamii nyengine kama Bilal Ibn Rabah, Salman Al-Fursi nk. Kwahiyo, madai haya ya watu wa dini za kiafrika hayana mashiko wala msingi wowote.

Kuhusu kwamba Uislamu ni dini ya "kuletewa", kitu kinacholetwa ni kutoka kwa watu wengine na kikawa hakina maana. Lakini imani ya Kiislamu ni kutoka kwa Allah (SWT) na Yeye (Allah) ndiye Muumbaji wa wanadamu wote. Ama dini ya Uislamu kuteremshwa kwa kuanzia kwa mtu fulani, hilo ni suala la
kutarajiwa na bahati hii ikaangukia kwa Muhammad bin Abdillah (swallahllahu alaihi wasalama) ambaye yeye alikuwa muarabu, lakini ujumbe aliopewa haukua kwa ajili ya waarabu tu, bali kwa wanadamu wote:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ

*"Wala hatukukutuma (ewe Muhammad) ila kuwa ni rehema kwa viumbe wote"*

Kuna madai kuwa kabla ya Uislamu na dini nyingine watu wa Afrika tulikuwa tunaomba katika imani zetu za asili na kujbiwa. Haya ni madai ya kuchekesha sana, ikiwa walinganizi wa imani za kiafrika hawakubali dini za wageni sasa, kwanini leo hawaombi mizimu yao na kujibiwa ili wakoloni waondoke na umasikini

uondoke Afrika? Uhakika ni kuwa mizimu haina uwezo wa kujibu chochote, bali mawazo ya mizimu ni uchache wa kufikiri.

إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ

***"Hawafuati ila dhana tu, wala hawakuwa ila wanatabiri tu (bila ujuzi wa hakika)"***

Madai ya dini kudhoofisha maendeleo ni madai ambayo hayajazingatia uhalisia, pia kwanini hawasemi kuwa waliokuja kupora maendeleo ya Afrika mpaka leo ni mabepari wanademokrasia. Waumini wa mizimu na dini za jadi wanapoacha kutaja waporaji halisi wa Afrika na kukimbilia dini ni wazi wanatumiwa na hao waporaji,wawe wanajua au hawajui. Je katika hii Afrika dini gani ipo ikulu inatawala kwa sheria za dini? Ili iwe hoja kwamba dini hiyo, imewafanya watu wa nchi hiyo kuwa maskini. Lakini ukweli na uhalisia watu wanatawaliwa na sharia za kibepari za kisekula.

Ama madai kuwa dini au Uislamu umekuja kufuta majina yetu ya asili. Ukweli ni kuwa Uislamu haujalazimisha mtu kubadili jina anaposilimu bali ni khiyari. Wasichofahamu hawa wapinga dini ni kwamba waarabu wapo Afrika kwa wingi na kwa karne na karne je ili waishi bara hili lazima waitwe kina "Lihenyuke"?

Uislamu unalazimisha kubadilisha jina kama litakuwa na maana mbaya haijalishi mwenye jina hilo ni mwarabu, mwafrika, mchina, muhindi, mzungu nk. lakini ikiwa mtu anaitwa "Sengiyunva" ikiwa maana yake ni nzuri halazimishwi kubadili jina.

Kukataa Uislamu kudai kuwa dini zimeleta vita na machafuko hii pia si hoja madhubuti. Kwa bahati mbaya hawataji hata vita moja au mfano wa vurugu hizo ambazo Uislamu umeleta. Mfano leo vita ya Congo, Ukraine na Urusi, Msumbiji, Angola, Vita vya Kwanza na vya Pili vya Dunia nk. Je sababu yake ilikuwa dini? Bali wapagani leo hii ndio wana ongoza dunia, na hata kama mtawala atakuwa si mpagani basi atatawalisha fikra na sheria za kipagani na sio za dini yake.

Kuhusu dini kuleta ukoloni na utumwa. Dini ya Kiislamu iliingia Afrika karne ya saba na hakukutokea utumwa wala ukoloni mpaka karne ya 18 walipokuja wakoloni mapagani baada ya kulipindua Kanisa huko Ulaya na kutangaza upagani wa kibepari. Na kama walitumia kanisa kusaidia mambo ya utumwa, basi hilo litakuwa jambo la kanisa sio Uislamu. Na haifai kuhusisha dini katika muktadha wa utumwa, bali uadilifu ni kutaja muhusika moja kwa moja nayo ni dini ya ukiristo.

Kwahiyo, hoja hizi za kupinga dini zinazolenga kupinga Uislamu hazina nafasi kwa upande wa Uislamu, bali zinaweza kuwa nafasi kwa upande wa dini nyingine, kwani Uislamu umetakasika na udhaifu wote uliopo katika dini nyingine.

Wafuasi wa dini hizi za jadi ambazo hazina hoja waachane mara moja na dini ambayo inashindwa hata kujitetea na waje katika Uislamu, dini ya haki inayokinaisha akili na kuwafikiana na maumbile ya mwanadamu.

Amma Waislamu wasichoke kujadiliana na wafuasi wa dini za jadi na wengine kwa njia ya kistaarabu kuwakinaisha kuhusu Uislamu. Kubwa na nyeti zaidi kwa Waislamu ni

**Inaendelea uk ... 8**

Mwenyezi Mungu.

Sayansi huelezea mada na sababu za kimada pekee, kwavile hakuna mada nyuma ya mada ndiyo imekuwa vigumu sayansi kufafanua chanzo cha mada na hivyo kuita mada ndiyo chanzo chenyewe.

Njia pekee ya kufahamu kilicho nyuma ya mada ni kufikiri kwenye tija (rational thinking) ambayo msingi wake mkubwa ni sababu (reasoning). Kwa kutumia fikra tunagundua kuwa mada pia ina chanzo (imeumbwa) kwa vile ni kitu na hii inalazimisha uhalisia kuwa Mwenyezi Mungu yupo.

Kutokuonekana si hoja ya kutokuwepo Mwenyezi Mungu

Hoja ya kuwa Mwenyezi Mungu hayupo kwa sababu haonekani kwa macho ni dhaifu sana. Mwanadamu ana akili uwepo wa vitu vingi bila ya kuwa na uwezo wa kuviona kwa macho mfano akili, roho,nk. bali kwa kuona athari zake tu.

Kimsingi uwepo wa kitu unathibitisha uwepo wa mmiliki wake au aliyekitengeneza. Mfano, mtu akinunua simu ya mkononi kutoka China ataamini kuwa simu ile haijajiibukia tu bali yupo aliyeitengeneza na ataitumia simu ile kwa kufuata maelekezo ya mtengenezaji hata kama hajamuona!

Hii pia inathibitisha kuwa Mwenyezi Mungu yupo Pamoja na kuwa haonekani, Yeye ni mtukufu sana na sio kiumbe.

Ama kwa upande wa Quran

**Inaendelea uk ... 8**

# Baadhi ya Visimamo na mabango Maeneo mbalimbali




Pichani: Wanaharakati ya Hizb ut Tahrir Tanzania maeneo mbalimbali ya Tanzania wakiwa katika visimamo na mabango nje ya Misikiti ya Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga, Pwani nk.yenye kaulimbiu : "KATAA DINI MSETO, UKIRISTO, UPGANI, MIZIMU, BAKI NA UISLAMU"

## Upagani—kutoka uk 4

ambacho nchi za Ulaya na baadae Marekani kumakinika na kuwa juu kwa mfumo wao wa kibepari. Nchi hizi zikatajirika zaidi kwa ukoloni na unyonyaji na zikang'ara kwa uvumbuzi wa sayansi zikapata nyenzo zaidi za kuubeba na kuusambaza mfumo wao wa ubepari na aqida yake ya 'usekula' ambayo inachukia na kuidharau dini kila mahala.

Mtazamo wa ubepari na wanafikra wake kuchukia dini ni jambo ambalo halikujengwa juu ya uadilifu. Kwa sababu wanafikra na wanamageuzi wake hawakusoma wala kutafiti dini nyengine, bali walitosheka na uzoefu wao na tareekh ya ukiristo ndani ya Ulaya kuhukumu dini zote kwamba ni uovu.

Harakati za upagani zimeshamiri na kufadhiliwa kimataifa na nchi za magharibi na Marekani ili kwanza kulinda matunda ya mapinduzi yao ambayo natija yake ni kuchukia dini. Lakini kubwa zaidi ni kupambana na Uislamu ambao ndio mlengwa mkubwa. Vita dhidi ya dini na ukanushaji wa dini zote ni guo la kujifichia tu, kinachokusudiwa hapa ni dini moja tu nayo ni Uislamu kwa kuwa ndio dini yenye mfumo kamili na tishio kwa mfumo wa ubepari.

Mabepari wanatapatapa katika kukabiliana na Uislamu, lakini hakuna watakalofanikiwa katika vita vyao hivi, ikiwa makomunisti wamepambana usiku na mchana kuzuiya na kudhibiti Uislamu kwa nguvu kubwa na kulifanya suala la kukanusha Muumba ni thaqafah katika kila sekta ya jamii, makazini, mashuleni, kwenye michezo kwa miaka 70, na hawakufanikiwa. Basi itawezekana vipi wafanikiwe mabepari?

وَإِنْ كَانَ مَكْرُهُمْ لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ (إبراهيم: 46).

…"*Na havikua vitimbwi vyao (kuwa na uwezo) wa kulindoa jabali" (TMQ Ibrahim: 46)*

## Imani za kijadi … *Kutoka uk .7*

kushiriki katika mchakato wa kurejesha tena dola ya Kiislamu ya Khilafah Rashidah ili kuja kuilinda kikweli aqida ya Uislamu, na kuuokoa ubinadamu na dini na fikra za kuchanganyikiwa ambazo leo ubepari unazipigia debe na kuzidhamini.

#DiniYaHakiUislamuTu

## Hoja za kiakili ..kutoka uk 7

Tukufu imetudhihirishia wazi kuwa binadamu na kila kitu kimeumbwa na Mwenyezi Mungu na Yeye ni wa enzi wa milele, alikuwepo kabla ya kila kitu na ndiyo chanzo cha ulimwengu, binadamu na uhai. Anasema Allah SWT:

أَوَلَا يَذْكُرُ ٱلْإِنسَٰنُ أَنَّا خَلَقْنَٰهُ مِن قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْـًٔا

Je! hakumbuki mwanaadamu ya kwamba tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote? (Maryam: 67)

****